Programu ya Makazi ya Hisani

Programu ya Makazi ya Hisani (Humanitarian Settlement Program - HSP) inatoa msaada kwa wahamiaji wa hisani ili kujenga ustadi na ujuzi wanaohitaji kuwa wanachama wa kujitegemea na kuwa wahusikaji wa jamii ya Australia.

Kushiriki katika HSP ni kwa hiari na huduma hutolewa kwa wateja kupitia mbinu wa usimamizi wa kesi unaoendana na mahitaji.

Watoaji huduma wa HSP huwasaidia wateja kupata matokeo katika maeneo yafuatayo kama msingi wa makazi ya mafanikio:

- Ajira
- Afya ya kimwili na kiakili na ustawi
- Elimu na mafunzo
- Ushiriki wa jumuiya na kujenga mitandao
- Makazi
- Kufaa kazi kwa familia na msaada wa jamii
- Kusimamia fedha
- Haki
- Huduma za lugha

HSP ina lengo la kufanya kazi pamoja na huduma nyingine za makazi na za kawaida. Ina lengo kubwa la kuwasaidia wateja kujifunza Kiingereza na kupata ujuzi muhimu wa elimu pamoja na ajira kwa kutambua kwamba matokeo mazuri katika maeneo haya husaidia wahamiaji wa hisani kuzoea kuishi katika maisha ya Australia.

Msaada unaotolewa chini ya HSP

Wasimamizi wa kesi wa HSP wanafanya kazi kwa kushirikiana na wateja ili kuendeleza mpango wa usimamizi wa kesi binafsi na kutoa huduma mbalimbali zinazofaa kulingana na mahitaji yao yaliyotambuliwa.

Huduma ni pamoja na msaada mapema wa utendaji kama:

- mapokezi kwenye kiwanja cha ndege
- makazi baada ya kuwasili na kuonyeshwa jinsi ya kutumia nyumba
- kupewa chakula na vitu vya muhimu mwanzoni
- msaada wa kujiandikisha na KiungoKati (Centrelink), TunzaAfya (Medicare) na benki
- kuangalia mahitaji ya mara moja ya afya
- maelekezo ya kufanya nini katika hali ya dharura na jinsi ya kupata huduma za kutafsiri
- kutambulishwa kwenye huduma za mahali.

Huduma nyingine zinazopatikana ili kusaidia wateja kufikia matokeo yao ya makazi hujumuisha:

- utoaji wa programu ya Kuzowesha maisha unaojenga ujuzi wa wateja kuhusu njia ya maisha na maadili ya Australia
- msaada wa kupata makazi ya muda mrefu
- msaada wa kupata huduma za kawaida, pamoja na huduma za afya na kusaidia familia
- uhusiano na vikundi vya jamii na shughuli za jamii
- msaada wa kujiandikisha na Programu ya Kiingereza kwa Watu Wazima Wahamiaji (Adult Migrant English Program - AMEP) na kuhudhuria masomo
- msaada wa kusajilisha katika elimu na mafunzo yenye kufaa na kutambua ustadi na sifa za kabla ya kuwasili
- msaada wa kushirikiana na huduma za ajira, kutekeleza mikakati ya ajira na kupata huduma za msaada kwa kuanzisha biashara.

Watoaji huduma wa HSP pia wanaweza kuwezesha kuweka maombi ya Huduma ya Ufasiri ya Bure (Free Translating Service - FTS) kwa wateja wanaostahili wa FTS ambao hawawezi kuomba kwenye mtandao.

Kutoka kwenye HSP inategemeana na wateja kufikia matokeo ya makazi yaliyotambuliwa katika mpango wao wa usimamizi wa kesi. Kwa wateja wengi, matokeo haya yatafikiwa ndani ya miezi sita hadi 18 ya kuwasili nchini Australia.

Huduma Maalumu na za Kina

HSP hutoa Huduma Maalumu na za Kina (Specialised and Intensive Services - SIS) kwa wahamiaji wa hisani na wamiliki wengine wanaostahiki viza ambao wana mahitaji magumu.

SIS inatoa msaada wa muda mfupi (kwa ujumla, hadi miezi sita) kwa wateja kuwasaidia kufikia huduma zinazofaa na kuendeleza ujuzi muhimu ili kusimamia mahitaji yao kwa kujitegemea.

Idara ya Huduma za Jamii (Department of Social Services - DSS) inapaswa kukubali pendekezo kwa mtu kupokea SIS. Kwa habari juu ya jinsi ya kufanya pendekezo, angalia - Jinsi ya kumtuma mtu kwa SIS.

Kupata HSP

Mtu anapotolewa mojawapo ya viza zifuatazo ili kukaa nchini Australia, hutumiwa na DSS kwa mtoa huduma wa HSP kufikia msaada chini ya HSP baada ya kuwasili nchini Australia.

- Viza ya Ukimbizi (Refugee) (daraja ndogo 200, 201, 203 na 204); na
- Viza ya Hisani Maalam (Global Special Humanitarian) (daraja ndogo 202) *

* Watu waliopewa viza 202 chini ya Mpango wa Usaidizi wa Jamii (Community Support Program - CSP) hawastahili kupata msaada chini ya HSP baada ya kuwasili nchini Australia wakati wanapopata huduma za makazi kutoka Shirika la Fadhili la Kukubaliwa (Approved Proposing Organisation). Habari kuhusu CSP inapatikana kutoka kwenye tovuti ya Idara ya Mambo ya Ndani (Department of Home Affairs) kwenye www.homeaffairs.gov.au. Kwa mujibu wa kibali cha DSS, washiriki wa CSP wanaweza kustahili kupokea SIS.

Ustahiki wa SIS

Kwa mujibu ya idhini ya DSS, watu wanaofanya viza zifuatazo wanaweza kustahili kupokea SIS chini ya HSP:

- Viza ya Ukimbizi (Refugee) (daraja ndogo 200, 201, 203 na 204); na
- Viza ya Hisani Maalam (Global Special Humanitarian) (daraja ndogo 202)
- Viza ya Ulinzi (Protection) (daraja ndogo 866) visa; na
- Viza ya Ulinzi wa Muda (Temporary Protection) (daraja ndogo 785), ya Hisani ya Kukaa kwa Muda (Temporary Humanitarian Stay) (daraja ndogo 449), ya Suala la Hisani ya Muda (Temporary Humanitarian Concern) (daraja ndogo 786) na Shughuli ya Kimbilio cha Salama (Safe Haven Enterprise) (daraja ndogo 790).

Wamiliki wa viza hizi wanaweza kustahili SIS kwa hadi ya miaka mitano baada ya kuwasili nchini Australia au hadi miaka mitano baada ya kupata viza zao nje ya nchi ya kustahili. Katika hali ya kipekee, kubadilika kunaweza kuonyeshwa kwa wakati huu na wamiliki wa daraja ndogo ya viza vingine. Waraia wa Australia hawastahili SIS.

Watu wanaostahiki SIS wanapaswa kuonyesha kuwa hawawezi kushiriki kwa kujitegemea kwa msaada wenye kufaa **na** kuathiriwa na vikwazo vingi au vigumu vinavyoweza kujumuisha:

- ulemavu
- masuala ya ustawi wa watoto na vijana
- mahitaji ya afya ambayo ni makali, ya kipeo, ya muda mrefu na/au kutosimamiwa
- uharibifu wa familia na/au uhusiano
- matatizo ya kisheria
- matatizo ya afya ya akili
- kutengwa kwa kijamii
- ukosefu wa makazi au utulivu wa makazi
- shida ya kifedha
- vurugu ya kinyumbani au ya familia

Jinsi ya kumpendekeza mtu kwa SIS

Shirika lolote au mtu yeyote anaweza kupeleka mtu kwa SIS, ikiwa ni pamoja na kujipeleka mwenyewe. Kufanya pendekezo, tafadhali jaza Fomu yaKupeleka SIS (SIS Referral Form) inayopatikana kwenye www.dss.gov.au.

Ikiwa huna hakika kama mtu anastahili SIS, unaweza kuwasiliana na DSS kwa msaada kwa kupigia simu 1300 855 669 (simu ya bure nchini Australia) au tuma barua pepe SIS@dss.gov.au.

Watoaji Huduma wa HSP

HSP hutolewa kwa niaba ya Serikali ya Australia na watoa huduma watano katika mikoa 11 ya mkataba nchini Australia

Mtoaji Huduma HSP	Jimbo	Mikoa/Mkoa ya mkataba	Mahali pa Makazi
Settlement Services International Limited	NSW	Sedni (Sydney); NSW Mikoani (Regional NSW)	Sedni (Sydney); Nukasel (Newcastle); Kofs Haba (Coffs Harbour); Armedeil (Armidale)
Australian Red Cross	NSW/ACT	Kanbera na mazingira yanayozunguka (Canberra and surrounds)	Kanbera (Canberra); Wulongong (Wollongong); Wagga Wagga; Albury
	WA	Australia Magharibi (Western Australia)	Perth
AMES Australia	VIC	Melbon (Melbourne); Viktoria Mikoani (Regional Victoria)	Melbon (Melbourne); Meldura (Mildura); Sheperten (Shepparton); Gilong (Geelong); Wodonga
	SA	Australia Kusini (South Australia)	Adeleid (Adelaide); Mlima wa Gambiya (Mount Gambier)
	TAS	Tazmania (Tasmania)	Hobart; Lornsesten (Launceston)
MDA Ltd	QLD	Brisben na mazingira yake (Brisbane and surrounds); Kwinsland Kaskazini (North Queensland)	Brisben (Brisbane); Gaold Kost (Gold Coast); Logan; Tuwumba (Toowoomba); Keanz (Cairns); Townsville
Melaleuca Refugee Centre	NT	Wilaya ya Kaskazini (Northern Territory)	Darwin

Mahali pa majengo ya watoa huduma wa HSP na habari ya mawasiliano yanapatikana kutoka www.dss.gov.au.

Maelezo zaidi

Ili kujifunza zaidi kuhusu HSP, na shughuli nyingine za makazi zinazoendeshwa na DSS, angalia www.dss.gov.au.